



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS TAMISEMI

HALMASHAURI YA WILAYA YA MUSOMA
(Barua Zote Zijibiwe kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya)



Kumb. Na. E 4/2/49

23 Mei, 2022

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Musoma anawatangazia nafasi za kazi za Dereva II na Katibu Mahususi III. Nafasi hizi za ajira zinatokana na Kibali cha ajira kutoka kwa Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa barua Kumb Na. FA.97/228/01/9 ya tarehe 13 Mei 2022.

1.0 DEREVA II NAFASI NNE (04)

2.1 MAJUKUMU YA KAZI

- a. Kukagua gari kabla na baada ya safari ili kubaini hali ya usalama wa gari.
- b. Kupeleka watumishi maeneo mbalimbali kwenye safari za kikazi.
- c. Kufanya marekebisho madogo madogo ya gari.
- d. Kukusanya na kusambaza nyaraka mbalimbali
- e. Kujaza na kutunza taarifa za safari zote katika daftari la safari
- f. Kufanya usafi wa gari na
- g. Kufanya kazi nyingine kadri atakavyoelekezwa na Msimamizi wake.

2.2 SIFA ZA MWOMABAJI

- a. Awe na elimu ya kidato cha nne
- b. Awe na Leseni daraja E au C1 ya uendeshaji magari ambayo amefanyia kazi kwa muda usioupungua mwaka mmoja bila kusababisha ajali.
- c. Awe amehudhuria mafunzo ya uendeshaji magari (Basic driving Course) yanayotolewa na Chuo cha mafunzo ya ufundi stadi (VETA) au chuo kingine
- d. kinachotambuliwa na Serikali.
- e. Waombaji wenyewe cheti cha majoribio ya ufundi Daraja II watafikiriwa kwanza.
- f. Awe na Namba ya Utambulisho wa Uraia kutoka mamlaka ya vitambulisho vya Taifa (NIDA)

2.3 MSHAHARA

Mshahara utalipwa kwa kuzingatia viwango vya Serikali TGS "B"

2:0 KATIBU MAHSUSI DARAJA LA III NAFASI NNE (4)

2.1: MAJUKUMU YA KAZI

- a. Kuchapa barua, taarifa na nyaraka za kawaida
- b. Kusaidia kupokea wageni na kuwasaili shida zao, na kuwaelekeza sehemu wanapoweza kushughulikiwa
- c. Kusaidia kutunza taarifa/kumbukumbu za matukio, miadi, wageni, tarehe za vikao, safari za Mkuu wake na ratiba ya kazi zingine zilizopangwa kutekelezwa katika ofisi anamofanyia kazi, na kumuarifu Mkuu wake kwa wakati unaohitajika.
- d. Kusaidia kutafuta na kumpatia Mkuu wake majalada, nyaraka au kitu chochote kinachohitajika katika shuguli za kazi hapo ofisini
- e. Kusaidia kufikisha maelekezo ya Mkuu wake wa kazi kwa wasaidizi wake na pia kumuarifu kuhusu taarifa zozote anazokuwa amepewa na wasaidizi hao
- f. Kusaidia kupokea majalada, kuyagawa kwa Maofisa walio katika sehemu alipo, na kuyakusanya, kuyatunza na kuyarudisha sehemu zinazohusika.
- g. Kutekeleza kazi zozote atakazokuwa amepangiwa na Msimamizi wake wa kazi.

2.2 SIFA ZA MWOMABAJI

- a. Awe na elimu ya kidato cha nne au sita
- b. Awe amehudhuria mafunzo ya Uhazili na kufaulu mtihani wa Hatua ya Tatu.
- c. Awe amefaulu Hatimkato ya Kiswahili na Kiingereza maneno 80 kwa dakika na awe amepata mafunzo ya Kompyuta kutoka Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali na kupata cheti katika program za Windows, Microsoft Office, Internet, E-mail na Publisher.

2.3 MSHAHARA

Mshahara utalipwa kwa kuzingatia viwango vya Serikali **TGS “B”**

3:0 MHUDUMU WA JIKONI/MESS DARAJA LA II NAFASI TATU (3)

3.1 MAJUKUMU YA KAZI

- a. Kusafisha vyombo vya kupikia
- b. Kusafisha vyombo vya kulia chakula

- c. Kusafisa meza itumiwayo kwa kulia chakula
- d. Kuwatayarishia wapishi/waandazi vifaa vya mpishi na mezani
- e. Kusafisha maeneo ya kulia chakula na kupikia
- f. Kuwasaidia waandazi wa wapishi.

3:2 SIFA ZA MWOMABAJI

- a. Kuajiriwa wahitimu wa kitado cha nne wenye uzoefu wa kazi kwa muda usiopungua miaka mitatu.

3:3 MSHAHARA

Mshahara utalipwa kwa kuzingatia viwango vya Serikali **TGOS "A"**

4:0 MASHARTI YA JUMLA

- a. Waombaji wote wawe Raia wa Tanzania
- b. Waombaji wote wawe na umri kati ya miaka **18** hadi **45**
- c. Maombi yaambatanishwe na vyeti vya taaluma, cheti cha kuzaliwa na Kitambulisho cha NIDA au namba ya NIDA.
- d. **Testimonials Provisional result, Statement of Result** hati za matokeo ya kidato cha nne na sita hazitatambulika.
- e. Kila Mwombaji aambatanishe maelezo binafsi "**CV**" yenye anuani na namba za simu na majina ya wadhamini
- f. Waombaji wote waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe kuwa vyeti vyao vimehakikiwa na kuidhinishwa na mamlaka husika ya **TCU** na **NECTA**.
- g. Maombi yote yatumwe kwa Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Musoma
S.L.P 344 MUSOMA.

5:0 MWISHO WA KUTUMA MAOMBI

Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe **05/06/2022** Saa **9:30 Alasiri**


Msongela N. Palela
MKURUGENZI MTENDAJI (W)
MUSOMA

